

KUMWINUA JUU KUTOKA KATIKA HISTORIA



Asante, Ndugu Neville. Habari za jioni, marafiki. Kweli ni... Ninahesabu haya kuwa ni majaliwa makuu, kuwa hapa maskanini, usiku wa leo, kuanza tena mfululizo wa mikutano ya siku tano usiku. Imekuwa muda tangu nilipokuwa na uamsho hapa maskanini. Hatukulitangaza kwenye magazeti, ama chochote kile, kwa kuwa tulijua hatungekuwa na nafasi ya kutosha kuwaketisha watu, kwa sababu ni ndogo, na kuketi kwetu ni vibaya sana. Lakini tutafanya yote tuwezayo kuwaketisha. Tulikuwa tunaenda kuchukua jumba la mazoezi la shule ya upili hapa, na tungeweza kuitangaza, lakini huko ni wakati wa shule sasa, na ni vigumu kupata.

² Nami nitaondoka hivi karibuni, nadhani, kwa misheni zangu na kadhalika, kuvuka bahari. Nami nilitaka tu tukusanyike pamoja ili kufanya ushirika mdogo na watu wote kabla hatujakwenda huko tena.

³ Mnajua, tunakutana, mara kwa mara, na wakati mmoja tutakutana kwa mara ya mwisho. Kwa hiyo tu—tunataka kuwa karibu sana tuwezavyo na Bwana na Neno Lake, na tunapona Neno Lake likijifunua Lenyewe, siku baada ya siku, siku baada ya siku. Nilifikiri ingekuwa vema ikiwa tungekuwa na—na mkutano mdogo hapa, ndipo basi tungewaomba wagonjwa.

⁴ Na nimeambiwa, siku moja, kwa ono ambalo Bwana alinipa, mwaka mmoja uliopita, nadhani, au labda zaidi kidogo. Ninayo yameandikwa katika kitabu nyumbani, juu ya kubadilika kwa huduma. Na wengi wenu ninyi watu mnaoketi hapa... Nisingesema wengi. Lakini kumbukeni tulipojenga maskani hii kwa mara ya kwanza, mnakumbuka ono lililotokea asubuhi tulipoliweka jiwe la msingi pale, aliposema, “Hii siyo maskani yako.” Lakini aliniketisha chini ya anga na kusema, akaniambia mambo mbalimbali ambayo yangetukia. Kama mnajua, angalieni hilo likitimia kama tu lilivyosemwa. Mnaona? Na daima imekuwa hivyo. Kwa hiyo, basi, nakaa nikijua yakini kwamba kile asemacho, ni Mungu, na hakina budi kuwa kweli.

⁵ Halafu basi wakati fulani uliopita, nilikuwa katika ono na nikaona he—hema kubwa. Loo, ilikuwa ni kitu kikubwa, kikubwa mno. Nami nilikuwa nikizungumza tu, na watu wengi walikuwa madhabahuni, nao kidogo walikuwa wakilia tu huku mikono yao imeinuliwa juu, kwa utulivu na upole. Mtu mzuri mwenye sauti nyenyekevu alikuja jukwaani na kusema, “Sasa wataunda mstari wa maombi wakati Ndugu Branham

akijitayarisha.” Nami nilikuwa nimesimama *hivyo*, bila shaka, mstari wa maombi ungekuwa mkono wangu wa kushoto. Nami nikauona umati wa watu ambao walionekana kufunika bloku moja ya mji au zaidi, ambao walikuwa wamesimama kwenye mstari. Kulikuwa na jengo dogo, jengo la mbao, ndani ya hema hili. Na kulikuwa na mwanamke aliyesimama pale, mwanamume, akiandika majina, nao watu walikuwa wakiingia kwa magongo na machela, na kutokea upande ule mwingine, wakitembea. Vema, nikashangaa ni nini kilitukia mle ndani. Ndipo yule Malaika wa Bwana, Ambaye mnaona picha yake hapa, alitoka kwangu, na kwenda moja kwa moja juu ya jengo lile dogo, na kusimama pale, kisha akashuka. Ndipo Sauti ikanena, na kusema, “Nitakutana nawe mahali pale.” Vema, sasa, nimeutazamia kwa hamu wakati huo.

⁶ Nimekuwa mbali, wakati fulani sasa, nikipumzika, kwa sababu ya kazi nyingi. Nimerudi.

⁷ Nayo wikendi iliyopita, kidogo tulikuwa na fundisho dogo la kanisa kwa siku tatu usiku hapa. Hiyo ni, Jumamosi iliyopita usiku, Jumapili asubuhi, na Jumapili usiku, kabla ya mkutano huu. Kwa namna fulani kanisa tulitikise liingie katika hali, ili tuweze kuendelea na mkutano huu unaokuja sasa. Na mara baada ya haya, Jumapili usiku utakuwa usiku wangu wa kuiaga maskani kwa muda fulani, nijuavyo mimi. Na sasa . . .

⁸ Basi ninamtumaini na kumwamini Mungu, kwamba wakati fulani katika wiki hii, kwamba ninataka kukitumia chumba hiki kidogo hapa kama chumba cha maombi. Na kuwaleta wagonjwa na wanaoteseka ndani, nione kama atakutana nami, na kuanza maskanini tena, kwenye huduma mpya. Hakika ningependa kuliona likitendeka. Sijui ni nini, marafiki zangu. Sina fununu itakuwaje. Lakini Yeye anayesikiliza sasa, ninatumaini ya kwamba kitakuwa kitu kingine zaidi cha kuwasaidia maskini watoto Wake, wagonjwa, wanaoteseka wa siku hizi. Ninamwahidi kwamba nitakuwa mwaminifu na mtiifu, na kujaribu kuwa mwaminifu zaidi kuliko nilivyokuwa kwa karama zingine ambazo ametoa. Na kama itatimia, itakuwa halisi kama vile zingine zimekuwa. Sasa hizo karama zingine zingali imara kama zilivyokuwa. Mnaona? Lakini ninatazamia jambo jipya kutokea sasa, na ninatumaini litafanyika hapa. Sasa, nilifikiri, labda usiku wa leo tungezungumza na kuona jinsi nilivyohisi.

⁹ Na jambo lingine nililotaka kufanya, nilitaka kujaribu kujua, tunapoingia kwa mara ya kwanza, kama ningeweza kumpeleka mke wangu mle, na kumwacha awe pamoja nami itakaposhuka mara ya kwanza, kuona kama itakuwa hivyo. Kama sivyo, basi, katika kuwapitisha wanawake, tutawaleta wawili kwa wakati mmoja, wanawake wawili kwa wakati mmoja, wakipita. Kwa hivyo sisemi kwamba itafanya kazi kwa moja ya njia hizo; ni kwamba tu mpate kujua, kwa sababu tayari

imesemwa kwamba tulikuwa tunatafuta kitu kipya kitokee, na ndivyo tunafanya. Lakini sasa sisemi kwamba Yeye aliniambia ingetukia. Mahali nilipoona katika ono palikuwa kwenye hema. Lakini, bila shaka, linaweza kutendeka popote, wakati wowote, kwa hiyo tunaitazamia.

¹⁰ Sasa tutajaribu kuwaacha mwondoke mapema. Ibada ya nyimbo, nusu saa, na ibada ya kuhubiri, na ibada ya madhabahuni, na kadhalika, kama saa moja, ambayo itafanya saa moja na nusu, ili watu waliosimama wasishikwe na mkakamao; na warudi tena kesho usiku.

¹¹ Sasa, kabla tu hatujafungua Neno hili la kale lililobarikiwa. Nasi tutawahakikishia, kamwe hatutasema lolote nje ya yale yaliyo ndani ya Hilo, maana Hilo ndilo msingi. Basi kabla hatujafanya hivyo, hebu na tuinamishe tu vichwa vyetu, kwa maombi mafupi.

¹² Mungu Mpendwa, tunaposimama usiku wa leo katika Uwepo Wako, na kutambua umbo letu dhaifu, kwamba sisi ni mavumbi tu ya dunia. Umetutoa sisi kama viumbe hai, ili kukuheshimu na kukutukuza Wewe. Nasi tunatambua ya kwamba maisha yetu na hatima yetu iko katika mikono Yako iliyobarikiwa. Nasi tumejikabidhi, kwa imani, mikononi Mwako, tukitumaini kwamba tutapewa hatima yetu ya Milele, kuishi na Wewe milele katika ulimwengu ulio bora zaidi, ambapo kamwe hatutakuwa na maombi kwa ajili ya wagonjwa na wahitaji. Hakutakuwa na machozi yatakayoanguka shavuni. Hakutakuwa na m—mtu dhaifu, mwenye makunyanzi atakayekuja huko. Lakini tutakuwa vijana huko, milele, na utukufu wa Mungu utakuwa juu yetu. Wala hatutahitaji uponyaji, kwa maana tutaponywa Milele, milele. Wakati kiumbe hiki tulicho sasa kitakapobadilishwa na kufanywa mwili kama mwili Wake wenye utukufu, ndipo tutakapomwona jinsi alivyo. Mpaka saa hiyo yenye baraka itakapofika kwa kila mmoja wetu kuja, tunataka kuweka juhudi zote tunazojua, kulitukuza Jina Lako kuu, kwa imani kama uliyotupa Wewe.

¹³ Ni katika mkesha wa kusanyiko hili dogo hapa katika mahali hapa pa ukumbusho, katika ukumbusho wa uamsho wa kwanza tuliufanya hapa. Na matendo makuu mno uliyotuonyesha kwa mkono Wako mkuu wenye nguvu. Kutoka hapa uamsho umeenea kwa kila taifa. Na ulimwenguni kote, usiku wa leo, mioto ya uamsho inawaka vilimani, na wanaume na wanawake wanaponywa magonjwa yao na maradhi, na wanakuja kumjua Mungu wa kweli na aliye hai. Ee Bwana Mungu, mmwage Roho Wako juu yetu usiku wa leo, Bwana, katika vipimo vikubwa.

¹⁴ Na kama ikikupendeza Wewe, Bwana, kama liko katika mpango Wako wa Kiungu, tungeomba, Ee Mungu, kwamba katika jengo hili uweze kuiweka kazini karama hii mpya, kusudi hawa waliokaa nyuma, kutoka hudumani, na wakawa

ni mashujaa wa maombi, wapate kuona, kwa mara ya kwanza, mkono mkuu wa Yehova ukitenda kazi kwa njia hii mpya (Tujalie, Bwana.), na kuwa washiriki wa hayo matunda. Tunaomba tu kwa unyenyekevu kwamba itajaliwa hapa, tukijua kwamba itakuwa mahali fulani, kwa sababu tunahisi kwamba ni katika majaliwa Yako makuu kufanya hivyo.

¹⁵ Sasa utubariki, Bwana, tunapofungua kurasa za Kitabu, Neno Lako takatifu lililobarikiwa. Roho zetu na ziwe wazi kumpokea, Bwana. Na ibada itakapofungwa usiku wa leo, nasi tunaelekea kwenye makazi yetu mbalimbali, na tuseme kama wale waliotoka Emau, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, usiku wa leo, alipokuwa akisema nasi njiani?” kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

¹⁶ Usiku wa leo nimechagua, kwa ajili ya kusomwa tu kwa Maandiko, vifungu vichache, kama mngenda kufungua, kwenye Kitabu cha Wafalme, Wafalme wa Kwanza, na mlango wa 18 wa Wafalme wa Kwanza. Nami nataka kuanza kusoma kutoka kifungu cha 17. Nami ningependa kuchukua basi, kwa ajili ya somo: *Kumwinua Juu Kutoka Katika Historia*. Sasa, ninyi mnaoliandika, huenda nikalinukuu tena: *Kumwinua Juu Kutoka Katika Historia*. Sasa kifungu cha 17 cha mlango wa 18 wa Wafalme wa Kwanza.

Ikawa, Ahabu alipomwona Eliya, Ahabu akamwambia, Je, Ni wewe, ewe mtaabishaji wa Israeli?

Akajibu, Mimi si mimi niliyewataabisha Israeli; bali wewe na nyumba ya baba yako, kwa kuwa mmeziacha amri za BWANA, na kwamba wewe umewafuata Mabaali.

Basi sasa upeleke watu, unikusanyie jamii ya Israeli katika mlima wa Karmeli, na wa wale manabii wa Baali mia nne na hamsini, na wale manabii wa Ashera mia nne, walao chakula mezani pa Yezebeli.

Basi Ahabu akawapeleka watu kwa wana wa Israeli wote, akawakusanye manabii pamoja katika mlima wa Karmeli.

Naye Eliya akawakaribia watu wote, akasema, Mtasita-sita katikati ya mawazo mawili hata lini? BWANA akiwa ndiye Mungu, mfuateni yeye: ikiwa ni Baali, haya, mfuateni yeye. Wale watu hawakumjibu neno.

¹⁷ Tunasimama usiku wa leo ukingoni, na kutazama yakitukia, na kufunguliwa, maonyesho mawili makuu. Na maonyesho hayo mawili makuu ni haya: mojawapo ni mwisho wa historia, na lingine ni mwisho wa wakati. Na watu wengi wakuu, kote katika nyakati, wametamani kuona majira haya ambayo sasa tunayakaribia. Na tunapoishi katika kutua huku kutukufu kwa jua linalopatikana na mauti na kupambazuka kwa Nuru ya

Milele, ninahisi kwamba tunaishi katika mojawapo ya enzi kuu ambazo mwanadamu amewahi kuruhusiwa kuishi, kwa sababu ni kumalizika kwa wakati na kuingizwa kwa Umilele. Historia inatwambia tu kile ambacho tumesoma, kile kimekuwako. Na mambo yajayo yako mkononi mwa Mungu. Nasi tunaona, siku hizi, ya kwamba hakuna historia nyingi sana inayoandikwa, kwa sababu sidhani itawahi kutumika.

¹⁸ Matukio haya mawili makuu yote yanapitia kwenye maji ya kina kifupi. Kwa mfano, . . . Jinsi tunavyoshughulikia hatari za kitaifa. Na usalama wa taifa unaingia kwenye maji yenye kina kifupi. Huku nikisafiri kote, ulimwenguni, inaonekana kana kwamba sio taifa letu pekee, lakini hakuna taifa linalojua kabisa la kufanya. Inaonekana kuna maasi kila mahali. Ninaingia Afrika, wote wanaogopa maasi miongoni mwa watu, na ukomunisti ukienea nchini. Ninaenda Uswisi, vivyo hivyo. Na mataifa mengine yote ambayo nimetembelea, inaonekana kuwa kuna vurugu kila mahali.

¹⁹ Sasa unajua, Bwana wetu alibashiri wakati kama huo kuja, kwamba kutakuwa na “machafuko kati ya mataifa, fadhaa za wakati, dhiki kati ya mataifa.”

²⁰ Nasi tumejaribu kila kitu kinachoonekana kuwezekana kibinadamu, kuufanya udumu kwa muda mrefu zaidi. Lakini ninaamini kwamba tunaishiwa tu. Siamini kwamba kuna kitu kingine chochote ambacho tunaweza kufanya kulihusu. Tuko tu mwishoni mwake. Tulijaribu kwa muda, kuwa na wafalme, na hawangefanikiwa. Kisha wakajaribu demokrasia; haifanyi kazi. Na tumejaribu . . . Wamejaribu madikteta, wala haifanyi kazi. Na kila moja inaonekana kuwa na kina kifupi zaidi, kila wakati. Sasa tunasimama kwenye wakati mkuu sana wakati jambo lolote linaweza kutokea. Inaweza kumalizika, katika muda wa dakika tano, ambapo kila taifa lingekuwa unga.

²¹ Na kama tuko kwenye wakati huo, Kanisa linapaswa kuwa wapi? Hatari kubwa!

²² Halafu, pia, tuna upeo wa hatari ya maisha ya nyumbani. Inaonekana kana kwamba maisha ya nyumbani yanaishia kwenye maji ya kina kifupi. Ilikuwa, nyumbani, kwamba baba, mkuu wa nyumba, angeketi chini asubuhi, naye angezungumza na familia yake, na wote wangetoa Biblia ya kale ya familia na kuisoma kidogo tu, na—na wote wanakusanyika mezani na kusali. Huoni hilo tena. Na siku ilipokwisha, naye mama akaosha vyombo, wote wangekusanyika na kusoma Biblia zaidi, na kuomba kabla ya kwenda kulala.

²³ Uhalifu wa vijana hakika ulikuwa ni—ni jambo gumu kupata katika siku hizo. Wavulana wote walienda shambani kufanya kazi. Na wasichana wakimsaidia mama kwa kuosha, chini kwenye kijito. Lakini, siku hizi, tunabonyeza tu kitufe kidogo na vyombo vyote vimeoshwa. Naye mama yuko ndani

ya gari na ameenda kwenye karamu ya kadi, ama huko nje akirandaranda mitaani. Na—nayo—kazi inafanywa na trekta wala hatuna chochote ila tu kundi la watu wazembe, wavivu.

²⁴ Nayo maisha ya nyumbani yamepuuzwa sana, mpaka Biblia imewekwa kando, mpaka wangelazimika kutafuta kwa saa moja ili kupata moja, katika nyumba nyingi Marekani. Wanaenda kanisani Jumapili asubuhi, kwa ajili ya dini yao, kwa yapata dakika ishirini. Na kama mchungaji atachukua kama dakika thelathini, anaitwa kwenye halmashauri. Ni nini? Maisha ya nyumbani yanaisha.

²⁵ Ilikuwa kwamba baba na mama walipendana na kuheshimiana na kuthaminiana. Naye alipokuwa mzee na mwenye mvi, na mwenye mikunyanzi, na maskini uso wake ulikuwa wote umebonyea, na miwani yake ikining'inia juu ya pua yake, baba alimpenda kama vile alivyompenda alipokuwa mchanga na mrembo.

²⁶ Lakini, siku hizi, simaanishi kuwa mkosoaji, lakini anapozeeka kidogo, yeye humbadilisha tu kwa mrembo mpya. Inaonekana kuwa hivyo, kama kubadilisha magari au kitu kingine. Inaonekana kwamba upendo ule halisi wa familia haupo tena. Kitu fulani tu kimetokea; maisha ya nyumbani yanaisha. Hatuna nyumba ya kale ya Marekani kama tulivyokuwa nayo, miaka mingi iliyopita.

²⁷ Kuna jambo lingine ambalo ningependa kusema, ambalo ni jambo lingine linaloisha, ni, urafiki unaisha. Haionekani kuwa tuna marafiki ambao tulikuwa nao. Nao marafiki tulio nao si marafiki waaminifu kama zamani. Ilikuwa, ninaweza kukumbuka, wakati mtu aliugua kwenye ujirani, kwamba kila mtu alikaribia na waliwasaidia katika kazi yao yote, na wakawasaidia kwa lolote lililoweza kufanywa. Wakaketi pamoja nao usiku kucha kwa wakati mmoja. Kama ninavyosema mara kwa mara, ni kweli, kwamba, ni vigumu kwetu kujua jirani amekufa mpaka tulione kwenye gazeti. Urafiki!

²⁸ Baba ana ufunguo wa nyumba, naye mama ana ufunguo. Na wote wawili wametoka wakaenda, nusu usiku. Nao watoto, hawajui walipo. Nao watoto wadogo wako pamoja na yaya. Na hivyo ndivyo maisha yanavyoishiwa.

²⁹ Je, unajua Biblia inatabiri mambo haya yote? Basi ni nini basi? Ni kwamba tunasimama mahali fulani tukiangalia mambo haya yakiisha.

³⁰ Hebu tuchukue maisha ya kanisa. Hapo ndipo yote yalipoanzia. Maisha ya kanisa yanaisha. Watu wanalichukulia tu kanisa, siku hizi, karibu kuwa kama sanamu, kama mti wa mzimu. Wanaenda wanaketi kanisani, dakika tano, na, "Nimetimiza dini yangu." Unatoa mchango wako mdogo, chochote kile, kumlipa mchungaji. Hazitoshi; wanaandaa chakula kidogo cha jioni, na kumlipia mchungaji. Na kama

hajaridhika, anasonga mbele mahali ambapo patamlipa ujira bora zaidi. Inaonekana kana kwamba mchungaji hajaitwa Kiungu tena. Inaonekana tu kwamba imeanza kuwa ni kupata riziki kwa mchungaji. Kwamba, popote watu wanapompa pesa nyingi zaidi, huyo anaenda huko. Haipaswi kuwa hivyo.

³¹ Inapaswa kuwa kwamba mtu aliitwa na Mungu kwa ajili ya umma. Na kama ilimbidi alale pale kama Eliya alivyofanya, juu ya mlima, kwenye kijito Kerithi, na kutarajia kunguru wamlishe, anapaswa kukaa mpaka huduma yake ya Kiungu imetimizwa. Haidhuru kama atapata senti moja, ama la, inapaswa kuwa wito wa Mungu, kwanza.

³² Lakini, inaonekana, imebadilishwa ikawa ni wito wa pesa, au wadhifa mkuu na kitu fulani kwenye utaratibu huo, ama kuwa mtu maarufu zaidi na kanisa kubwa zaidi, ama kitu kama hicho.

³³ Na halafu kanisa, mle ndani, wameachilia. Wanaanza kuisha. Angalia tu likijifunua.

³⁴ Sasa bado nina umri wa chini ya miaka hamsini. Na ninaweza kukumbuka nikienda kwenye kanisa la Baptisti na makanisa ya Methodisti, na kuwaangalia katika uamsho wa mtindo wa kale, wakati wangepaza sauti na kumsifu Bwana, na kutembea huku na huku kwenye marefu ya kanisa na kuwashawishi wenye dhambi waende madhabahuni. Huoni hilo mahali popote tena. Walikuwa wakifanya mikutano ya maombi ya mtindo wa kale wakati wa uamsho, naye mwenye dhambi katika ujirani, mvulana au msichana, na hao akina mama wakongwe na akina baba wangeomba kwa bidii sana hata wangeomba sadikisho juu ya watoto hao, nao wangeshuka madhabahuni, na hapo wamjie Kristo.

³⁵ Lakini huoni hilo tena. Inaonekana kama inapita kwenye maji ya kina kifupi. Haionekani kamwe kama inapaswa kuwa hivyo.

³⁶ Na basi ilikuwa kwamba karibu makanisa yote, miaka kadhaa iliyopita, wakati wangukuwa na uamsho katika kanisa moja, makanisa mengine yote yangeshirikiana. Nao wangeingia na kusaidia, na kuwatuma washiriki wao huko, na kufunga makanisa, na kufanya uamsho. Hulioni tena.

³⁷ Sasa nini kimetokea? Na utafanya nini kulihusu? Ni kutimizwa tu kwa Neno la Mungu aliye hai. Nazo zinaelekeza, mbao hizo mbili: moja ya hizo, kuisha kwa wakati; na huo mwingine, Kuja kwa Bwana Yesu. Kwa maana Roho Mtakatifu alinena waziwazi na kusema, "Siku za mwisho makanisa yatakuwa makaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wasiopenda kufanya suluhu, wasingizaji, wasiojizuia, na wenye kuwadharau walio wema." Kwa hiyo ikiwa Biblia imetabiri mambo kama hayo kuwa, tunawezaje

kutazamia jambo lingine isipokuwa hilo kutukia? “Wenye mfano wa utauwa, bali wakikana Nguvu zake.”

³⁸ Pitia taifa hili leo, mataifa yetu, utafute wachache wa waaminio wanaoamini; ninamaanisha, waaminio halisi wanaoamini kwamba Yesu Kristo kweli yu hai. Unaona, wamelifanya kanisa kuwa sanamu tu. Tumepitia hayo, siku chache zilizopita, katika mafundisho yetu. Tunalitupia kanisa Katoliki, sanamu zao, na kuisujudia wanapopita karibu na kanisa. Nao Waprotestanti ni wabaya vivyo hivyo, kwa hiyo wanaenda huko mara moja moja. Na labda baadhi yao huenda mara moja kwa mwaka, na hiyo ni kwenye Pasaka.

³⁹ Nilimsikia mhudumu hapa si muda mrefu uliopita, mjini, ambaye alitoa matamshi haya. Alisema, “Niliwaaga watu wangu wote, kwenye asubuhi ya Pasaka, ‘Krismasi njema.’” Kasema, “Sitawaona tena hadi Krismasi au Pasaka ijayo. ‘Krismasi njema!’”

⁴⁰ Na tunaposimama hapa, tukitazama mambo haya yakifunguka, na kila mmoja wetu wanadamu, na tunajua ya kwamba jambo fulani halina budi kutukia. Haiwezi tu kuendelea hivi.

⁴¹ Kila mtu hana wakati wa kusimama dakika tano. Wako tu kwenye kusukuma na kukimbia, na haraka na msongamano, kupitia barabarani. Wakati watoto walipokuwa wakipanda barabara kuu alasiri hii, nilikuwa nikija. . . Au, alasiri, ndivyo ilivyokuwa. Nilikuwa nikitoka New Albany. Na huyu hapa mama anakuja akipitia barabarani, miongoni mwa watoto hao, karibu. . . katika eneo la maili ishirini, yapata maili sitini ama sabini kwa saa, haraka tu kama alivyoweza kutimua mbio. Kwani anaenda wapi? Katika dakika chache, nilisema, “Unaonaje kuhusu hilo?” kwa mtu aliyekuwa pamoja nami. Hapa yanakuja mbio magari mengine mawili, kama mashindano ya magari, moja kwa moja miongoni mwa watoto hao. Kupitia njia yetu pale tunapoishi, asubuhi, ni kama uwanja wa mbio za magari; inawabidi kuharakisha kwenda nyumbani kuosha vyombo, ama kumsikiliza Arthur Godfrey, ama chochote kile. Kwani unaenda wapi? Kuna nini? Jambo ambalo limevuruga kitu hicho chote, ni kwa sababu wanaume na wanawake wamekuwa wenye kuupenda ulimwengu huu wa sasa. Jambo kuu, linalopaswa kuwa, lingekuwa ni kuja nyumbani kusoma Biblia na kuchukua muda kuomba.

⁴² Ninamfikiria mamake John Wesley, Susanne. Alikuwa mama wa watoto kumi na saba. Naye alikuwa na wakati wa kutumia, nadhani, ilikuwa ama saa mbili ama tatu kila siku katika maombi. Na kuwalea na kuwatunza watoto kumi na saba, ambao walimleta mmoja wa wahubiri wakuu zaidi ulimwenguni, na mmoja wa waandishi wakuu sana wa nyimbo wa siku hizo,

Charles na John. Kwa sababu, alichukua muda kumtumikia Mungu, na si kujihusisha na mambo ya ulimwengu.

⁴³ Na tulipoona msingi wetu wa taifa letu, msingi wa nyumba yetu, msingi wa kanisa letu, ukizama, basi, ndugu, tufanye nini? Basi, nataka kusema hivi. Loo, laiti ningelikuwa na sauti ambayo ningeweza kuitoa kwa ulimwengu! Tuna msingi imara uliosalia, na huo ni Neno takatifu lililobarikiwa la Mungu, Biblia. Kwa maana mbingu zote na nchi zitapita, lakini Neno la Mungu halitapita kamwe. “Na juu ya Mwamba huu,” Mungu alisema, “Nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu haiwezi kulishinda.”

⁴⁴ Kwa hiyo ni upendeleo wenye baraka jinsi gani kwetu sote, kunyosha mkono na kuichukua Biblia nzuri ya kale ya Mungu, na kufungua kurasa, na kujua ya kwamba tunasoma Ukweli moja kwa moja. Na kuona ya kwamba nyakati hizi zilitukia katika siku zilizopita, kwa maana inanena juu ya Mungu wa kihistoria. Na njia pekee ambayo tutawahi kuwa, kukabilia na njia hizi, ama ku—kuingia mstarini, ni kumwita, kutoka katika historia, huyo Mungu wa kihistoria. Kwa maana katika siku zote, katika yale maangamizi yaliyotangulia ile gharika, kabla ya kuja kwake Kristo, na katika matukio mbalimbali, Yeye hashindwi kamwe, anapoitwa. Yeye yuko sawa kila wakati.

⁴⁵ Ninawazia wakati sasa, ambapo taifa lilikuwa utumwani. Ilikuwa ni Israeli. Nao walikuwa kule Misri, wakapewa kazi ngumu na kuteswa, wapate kuwatumikia Wamisri. Ilionekana kana kwamba kila mtu alikuwa amekuwa baridi. Je, ulijua Israeli ilikuwa Misri mara mbili ya muda ambao Marekani imekuwa taifa? Hatuna zaidi ya miaka mia moja na hamsini au sabini, kitu kama hicho. Nao walikuwa miaka mia nne na ishirini utumwani, ama kule Misri. Lakini ilifika wakati, ambapo ilionekana kana kwamba matumaini yote yametoweka.

⁴⁶ Lakini kulikuwa na mwanamume mmoja na mwanamke walioonekana kuwa na imani katika Mungu wa kihistoria ambaye alinena na Ibrahimu katika wakati wa shida, nao waliamini wangeweza kumwita Naye angejibu. Na huyo alikuwa Ham-...Amramu na Yokebedi, mke wa Ham-...Amramu, mama na baba wa Musa. Na kama vile hapa, wakati fulani uliopita, nilikuwa nikihubiri na kutoa mfano mdogo wa jinsi ambavyo Amramu angerudi nyumbani usiku, naye angesema, “Yokebedi, nimechoka sana.” Na vichapo vipya mgongoni mwake, kutoka kwa mje—mjeledi wa mnyapara.

⁴⁷ Naye mama angekaa chini kwa subira, labda, na kuosha ma—mahali hapo, na kulia na kusema, “Loo, Amramu, je, hakuna jambo linaloweza kufanywa?”

⁴⁸ Ningemsikia akisema, “Loo, mpenzi, kama ungalikuwa pamoja nami leo, na kuwaona wakiwapiga hao wavulana, wakijaribu kukokota mizigo hiyo. Lakini walikuwa katili.

Waliwatendea kana kwamba walikuwa ni wanyama. Na hao ni vijana wetu wa Israeli. Je, hakuna kitu kinachoweza kufanywa?”

⁴⁹ Hayo ndiyo ninashangaa sasa. Kuwaona wavulana wetu vijana matineja, ambao watakuwa wanaume na wanawake wa kesho, matineja wetu siku hizi. Nywele zimeshuka shingoni mwao, na suruali zimefungiwa kwenye nyonga zao, huku bastola imehomekwa ubavuni mwao, sigara pembeni mwa vinywa vyao. Itakuwaje? Ungali ni utumwa chini ya ibilisi. Je, hakuna kitu kinachoweza kufanywa?

⁵⁰ Naye Amramu, labda mmoja tu wa wale wa pekee wa hilo taifa, ambao wangepanda vipandio vidogo, bila kujali jinsi alivyokuwa amechoka. Pale, kila usiku, angemwita Mungu wa Ibrahimu, Yule ambaye alikuwa amegundua kwamba alimjia Ibrahimu, na kumjia Ayubu, na kuja kwa Isaka, na kumjia Yakobo, wakati wa taabu. Na, hakika, kama Yeye angekuwa ni Mungu katika siku zao, Yeye angekuwa Mungu katika siku hiyo.

⁵¹ Na kama Yeye alikuwa Mungu katika siku za Musa, Yeye ni Mungu siku hizi. Anahitaji tu kuitwa kutoka kwa historia, na kuitwa kwenye eneo la vita.

⁵² Nami ninaweza kumwona Amramu, usiku baada ya usiku, haidhuru amechoka jinsi gani; hiyo ilithibitisha imani yake katika Mungu huyo.

⁵³ Lakini, siku hizi, watu, wasipopata kila kitu wanachoomba, mara ya kwanza wanapoomba, wanaonekana kufikiri kwamba amekufa. Tunachohitaji ni wanaume na wanawake, siku hizi, wenye roho ya ushujaa, wanaume na wanawake ambao wameazimia kushikilia, mpaka watakapomwona Mungu ambaye kweli yu hai, akiingia kazini, ambao hawatachukua “la” kama jibu. Wameamua kubaki nayo. Ikiwa ni wagonjwa, na daktari amesema hawawezi kupona, hata hivyo kitu Fulani ndani yao kinawaambia watakuwa wazima. Wanashikilia, haijalishi ni nini kinatokea! Je, umejiunga na makanisa ya ulimwengu wa madhehebu, baada ya kumalizia nguvu zako zote kwa kutembea kutoka mahali hadi mahali, na bado hupati faraja? Kungali kuna Mungu anayejibu maombi na kuokoa kutoka kwa dhambi.

⁵⁴ Na kama tunavyoweza kumwona, Amramu, katika usiku huo wenye uchovu, akivuja damu mgongoni, akipanda vipandio tena, mpaka saa nane na saa tisa asubuhi, akiomba, na kuonekana kana kwamba anazungumza tu na upepo. Ndani ya moyo wake wa Kiyahudi paliwaka imani ambayo hakuna pepo za shaka zingeweza kuizima.

⁵⁵ Hao ndio aina ya wanaume na wanawake tunaohitaji wajitokeze jukwaani leo. Kama hatajibu usiku wa leo, atajibu kesho usiku. Asipojibu mwaka huu, atajibu mwaka ujaar. Kwa maana, Yeye ni Mungu; si mungu *fulani*, bali *yule* Mungu.

56 Nasi tunamwona, usiku baada ya usiku, wakati Amramu akipanda vile vipandio. Naye Yokebedi angemjia na kusema, “Amramu, mpenzi, umekuwa hapa juu ukiomba usiku kucha. Kwa nini usiwaambie tu baadhi ya wavulana mahali unapofanya kazi, na kuwaacha waombe kidogo?”

57 “Naam, mpenzi, vipi kama hawatafanya hivyo? Mtu fulani hana budi kulifanya. Mtu fulani hana budi kuomba vya kutosha.”

58 Hivyo ndivyo kila Mkristo anavyopaswa kujisikia usiku wa leo; si kumngoja mtu mwingine, bali kuchukua mstari wa mbele, sisi wenyewe, na kuendelea. Ikiwa tunaamini Biblia kuwa ni historia, pia ni Kitabu cha unabii kinachosema ya kwamba Mungu yeye yule atafufuka katika siku za mwisho. Na wakati Wake wa kuja jukwaani umewadia.

59 Hilo ndilo Amramu alijua. Kwamba Musa alikuwa ametabiri... Au, si Musa. Samahani. Ibrahimu alikuwa amepewa ahadi na Mungu huyu wa historia, Ambaye hakuwa amejibu maombi kwa muda wa miaka mia nne, kadiri tulivyo na kumbukumbu. Lakini Yeye alitoa ahadi ya kwamba angewatoa.

60 Na, inaonekana, tumekuwa na Mungu mnyamavu kwa muda mrefu, lakini wakati umefika ambapo Yeye atajitokeza jukwaani.

61 Usiku mmoja Amramu alipokuwa ameomba, labda, kwa miaka kadhaa. Na nywele zake sasa zilikuwa zikiingia mvi, wala hakuna ukombozi, lakini mambo yakizidi tu kuzorota. Usiku mmoja alidhamiria sana. Ndivyo tunavyopaswa kufanya; tudhamirie kabisa. Alisema, “Mungu, uliahidi hili. Nasi tumelitazamia. Nasi tunaona ishara zote hapa, na wakati umekaribia. Wakati umewadia Kwako kufanya jambo kulihusu.”

62 Akiwa katika maombi mazito, akiomba kwa moyo wake wote, alitazama, akiwa amesimama pembeni. Akapangusa macho yake na kutazama tena. Hapo alisimama Malaika mwenye upanga uliochomolewa. Akasema, “Ukombozi unakuja. Nawe utamleta mwana ulimwenguni, naye ndiye atakayewakombo.” Unaona?

63 Mungu hujibu maombi kila mara, sivyo? Kama tukishikilia tu!

64 Musa, alipokuwa amewaongoza wana wa Israeli, kwa uaminifu, hata jangwani, akafika mpaka Bahari ya Shamu. Na milima upande mmoja, na majangwa upande mwingine, na jeshi la Farao *huku*, na Bahari ya Shamu mbele yao. Nao walikuwa wamenaswa katika rasi ndogo. Ilionekana kana kwamba hata maumbile yangepiga kelele. Itakuwaje? Wamekwisha. Jeshi la Farao, kwa makumi ya maelfu, kuwaponda-ponda.

⁶⁵ Lakini watu walifanya nini? Walianza kunung'unika na kulalamika. "Loo, afadhali tungelibaki mahali petu tulipokuwa."

⁶⁶ Lakini kulikuwa na mmoja kati ya watu hao, ambaye alikuwa na mwali wa imani ya Mungu ukiwaka moyoni mwake, ambaye aliamini kwamba Mungu wa kihistoria angeweza kujitokeza jukwaani katika hali yoyote ngumu. Musa alisimama akiwa amemwinulia Mungu mikono yake, na akaomba mpaka Mungu wa historia akajitokeza jukwaani kuwa Mungu katika siku hizi. Naye akaifungua njia, nao Israeli wakapitia majini, juu ya nchi kavu.

⁶⁷ Loo, haikuwa muda mrefu baadaye, mpaka Yoshua alipokuwa ameliongoza kundi lile lile, ama watoto wao, hadi Yordani. Na ilikuwa katika mwezi wa Aprili wakati mito yote inafurika, na Yordani ilikuwa mara tano ya ukubwa wake. Ilionekana kana kwamba kiongozi yeyote mzuri wa kijeshi angewaongoza tofauti na hivyo. Na ilikuwa wakati uo huo, wakati hapakuwa na uwezekano wa kuivuka. Lakini Yoshua akakumbuka kulikuwa na Mungu wa kihistoria, miaka arobaini kabla, aliyeifungua Bahari ya Shamu, naye akamwita Mungu huyo. Ndipo huyo Mungu akashuka katika nguvu kuu, naye akawa Mungu katika upeo wa hatari ya sasa, na kuifungua Yordani na kuwavusha.

⁶⁸ Ilikuwa miaka mingi baadaye, wakati somo letu, usiku wa leo, usomaji wetu wa somo, wakati Elisha alipokuwa ameona laana ya taifa hilo, naye alikuwa juu mlimani, na kwa mamia ya miaka hapakuwa na maombi yaliyojibiwa katika Israeli. Hata hivyo, Elisha alijua kwamba kulikuwa na Mungu wa historia ambaye angejitokeza jukwaani. Naye akawapa changamoto walimwengu wasioamini na kusimama mbele ya Mungu huyu na kuona ni yupi angejibu kwa moto. Naye Mungu ambaye angeweza kuwalinda wana wa Kiebrania kutoka kwenye tanuru ya moto aliteremsha moto na kuiteketeza dhabihu.

⁶⁹ Haikuwa muda mrefu pia baadaye wakati mtu mmoja alikuwa amekufa, jina lake Lazaro. Na kulikuwako na Mungu ambaye alikuwa angali anaishi, ambaye angeweza kumpeleka Henoko Nyumbani bila hata kuona mauti, na kumtwaa Eliya juu ya gari la farasi wa moto. Naye aliitwa jukwaani, katika saa ya giza ya mauti, Naye akatenda jinsi tu angefanya wakati wowote. Hata hivyo, Yeye alikuwa ni Mungu wa historia, lakini aliinuliwa juu kutoka kwa historia hadi kwenye upeo wa hatari ya sasa.

⁷⁰ Ilikuwa huko chini kwenye lango la Yeriko ambapo kipofu mmoja aliketi kando ya barabara, akilia. Matumaini yote yalitoweka. Hakuna madaktari wangeweza kumsaidia chochote. Pesa zake zilikuwa zimekwisha. Hakuna kitu chochote kilichobaki kwake isipokuwa kukaa hapo na kuota kwa siku chache, hadi kifo kingekuwa faraja tamu. Basi siku moja,

akishuka njiani, Mungu wa historia alijitokeza jukwaani, katika hatari ya sasa. Mungu akayafungua macho ya huyo kipofu.

⁷¹ Yuko katika nyumba ya Yairo, ambapo madaktari walikuwa wameshindwa, naye akamrudisha huyo msichana mdogo... apate kufa. Nayo mauti yalikuwa yameingia na maafa yake machungu, na kumchukua mtoto wa pekee, pale nyumbani, msichana mdogo wa miaka kumi na miwili, na kumlaza juu ya kitanda. Wakati mhubiri mdogo aliyevunjika moyo alipolazimika kuacha dhehebu lake na marafiki zake wote, lakini alikumbuka kwamba kulikuwa na Mungu wa historia ambaye angeweza kuwafufua wafu. Naye akaenda kumtafuta.

⁷² “Tafuteni, nanyi mtapata; bisheni, nanyi mtafunguliwa; ombeni, nanyi mtapewa.” Angali ni Mungu yeye yule.

⁷³ Wakati Mungu huyu, akikaa katika mwili uitwao Yesu, Mwana wa Mungu, alipoitwa jukwaani, aliitwa juu kutoka katika historia, Mungu Yule ambaye angeweza kuwafufua wafu katika Agano la Kale, kurudisha uhai kwa mtoto mchanga aliyekufa kupitia kwa nabii. Mungu huyo hawezi kufa. Yeye ni Mungu wa Milele.

⁷⁴ Mtoto huyo akiwa amelazwa pale kitandani, alijinyoosha. Na maskini Yairo akijua ya kwamba yule Mshunami alirudishiwa mtoto wake mchanga, akasema, “Mungu huyo wa historia, kama angaliweza kuitwa kutenda kazi, Yeye ni Mungu yeye yule leo.” Na akichunguza-chunguza, alikuwa amesikia habari za Mtu fulani—Mtu aliyedai kuwa na nguvu, na huyo alikuwa ni Yesu wa Nazareti, ambaye wote walimchukia. Lakini akamwita jukwaani, kwa maana Yeye alikuwa ndiye mwakilishi wa karibu sana wa Mungu ambaye angeweza kumpata siku hizo, Mungu wa Mungu aliye hai. Basi alipoitwa jukwaani, na Mungu wa kihistoria akaitwa, alitenda vile vile alivyofanya alipozungumza na Eliya juu ya mtoto huyo aliyekufa.

⁷⁵ Acha niseme hasa zaidi leo, ndugu yangu, dada, katika siku hii ya sasa wakati hatari, na wakati kansa inaula ulimwengu, na magonjwa ya kila namna; Mungu yeye yule wa kihistoria aliyemtakasa mwenye ukoma, akawaponya wagonjwa, na kuwafufua wafu, ndiye Mungu yeye yule leo. Anangojea kwa hamu watu Wake wamwite kwenye jukwaa la utendaji.

⁷⁶ Yule ambaye angeweza kumsamehe kahaba kwa kufanya uzinzi mara saba kwa siku; Yeye ambaye angeweza kumtakasa mwenye dhambi mchafu sana na kuwafanya kuwa weupe kama yungiyungi; Mungu yeye yule wa historia anaishi leo, kusafisha kila moyo mweusi wa dhambi na kutokuamini.

⁷⁷ Kuna mtu aliyekuwa na mvulana mwenye kifafa siku moja, naye akampeleka kanisani, nao wanafunzi wakacheza na kupiga mayowe karibu naye, kwa muda, wala haingefaa chochote. Lakini bado kulikuwa na Mungu wa historia ambaye aliishi. Alikuwa amedhamiria kumpata. Akamwona akishuka

mlimani, akamkimbilia, akasema, “Bwana, unihurumie. Pepo amemchukua mtoto wangu, naye hudhoofika na kuanguka motoni.”

⁷⁸ Yesu akasema, “Ninaweza, ikiwa unaamini.” Kama unaamini nini? Kama unaamini kwamba Mungu wa historia angali hai leo. Ndipo akaitwa jukwaani, nacho kifafa kikamwacha huyo mtoto.

⁷⁹ Mungu yuyo huyo anaishi leo; wakati makanisa yameshindwa, wakati siasa imeshindwa, wakati kila kitu kingine kimeshindwa, na mwanadamu ameshindwa, na kila kitu kimeshindwa. Mungu hawezi kushindwa. Yeye ni Mungu wa Biblia hii ya kale, yenye ngozi nyeusi. Ahadi Yake ni ya kweli kama ilivyopata kuwa. Na ni wakati ambapo watu Wake walimwita, wakamwinua kutoka katika historia. Kwa kuwa imeandikwa, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele.” Yeye ni Mungu wa kihistoria, na Yeye ni Mungu wa wakati huu.

⁸⁰ “Na katika siku za mwisho,” Yeye alisema, “Nitamwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili, na ishara na maajabu yatafuatana na hao waaminio; kwa maana kwa Jina Langu watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya; wakishika nyoka, au kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru; na wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

⁸¹ Huyo alikuwa ni Mungu wa kihistoria aliyetoa ahadi, nasi ndiyo watu siku hizi wa malisho Yake. Sisi ni kondoo wa zizi Lake, Naye anatungojea tusimame na kumwita jukwaani. Mwrite jukwaani. Mwone akianza kutenda kazi. Mwone akifanya makuu. Mwone akifanya jambo ambalo wanadamu watalistaajabia na kukuna vichwa vyao, wala wasielewe jambo hilo. Yeye ni Mungu wa kihistoria, na Mungu wa siku hizi. Anangojea kuitwa atoke katika historia.

⁸² Tusimwangelie Yeye. . . Je, Mungu wa kihistoria atatufaa nini ikiwa Yeye ni Mungu wa kihistoria tu? Je, Mungu wa kihistoria angaliwafaa nini Amramu na Yokebedi? Mungu wa kihistoria angemfaa nini Musa? Mungu wa kihistoria angemfaa nini Lazaro? Mungu wa kihistoria (angemfanyia) angemfaa nini kipofu Bartimayo langoni? Pia Mungu wa kihistoria angekufaa nini, usiku wa leo, kama si Yeye yule leo?

⁸³ Ni yeye yule leo. Anatusamehe dhambi zetu zote, na kuyaponya magonjwa yetu yote. Mungu wa kihistoria, aliyelitwa kutoka katika historia, Yeye ataangaza katika siku hii ya Nuru. Ati nini? Wakati unapomalizika, wakati siasa zinaisha, wakati maisha yanaisha, wakati kila kitu kinakaribia mwisho wake, Yesu anakuja kwenye Nuru. Wakati kila kitu kimekutana na maangamizi yake, Yeye bado anang’aa, “Ninyoro ya Bondeni, Nyota ing’aayo ya Asubuhi.”

⁸⁴ Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Mwrite tu Mungu wa kihistoria, na umwone akiwa Mungu wa sasa, aliyeinuliwa juu

kutoka katika historia, apate kuangaza tu kama alivyofanya wakati huo. Atafanya vivyo hivyo. Atafanya vivyo hivyo. Atasamehe vivyo hivyo. Ataponya vivyo hivyo. Huruma Zake ni zile zile. Hiari Yake ni vile vile. Na Nguvu Zake ni zile zile. Yeye ni yule yule. Anangojea ninii yetu. . .

⁸⁵ Huwezi kumwita kwa midomo yako. Haji kwa maneno matupu. Anakuja kwa imani. Wakati imani yako; sio maombi yako marefu, kuchoka kwako.

⁸⁶ Lakini Yeye huja kwa hiyo imani ndogo, hafifu iliyo chini kabisa ndani ya nafsi yako, inayoweza kushikilia na kusema, “Kitu hicho kidogo ambacho kimekuwa, kilinileta kwenye maskani hii usiku wa leo, kinaweza kuiangazia roho yangu upya, kinaweza kunipeleka mbali na hapa, kuwaka moto na kuimba, kama tu ndege wa angani.” Kwa nini? Yeye ni Mungu wa kihistoria na Mungu wa siku hizi. Anangojea kuitwa. Mwiteni Bwana. Atawasikia. Semeni Naye, kwa zaburi. Mwombeni na kumwamini. Atajibu.

⁸⁷ Na maneno haya nasema, katika kufunga. Hiyo ndiyo sababu ya mkutano huu, usiku wa leo. Hiyo ndiyo sababu mkutano huu umeanza. Ninaamini ya kwamba Mungu aliyeniambia, miaka ishirini na saba iliyopita, tulipoweka jiwe hili la msingi kule, kwamba ningehubiri Injili ulimwenguni kote. Alilitimiza. Walipocheka na kusema, “Kwani unaenda wapi, Billy, na elimu yako ya darasa la saba?”

Nilisema, “Ninaenda katika Jina la Bwana Yesu.”

⁸⁸ Nilipohubiri mahubiri yangu kabla ya kuondoka, miaka kumi na mmoja iliyopita, kwenye mimbara hii, na Bibi Gertie anayeketi pale, akaimba huo, *Amini Tu*. Nalo lile jitu kuu likasimama kule, kama nilivyohubiri, Daudi na Goliathi. Kulikuwako na sayansi na ulimwengu mkuu unaojulikana, kuhukumu uponyaji wa Kiungu na kuutia aibu. Na kila mtu akiniambia, “Kijana, utaingia wazimu huko nje. Watakutupa gerezani. Watafanya *hivi, vile*, ama *vinginevyo*. Lakini Mungu wa historia alikuwa amejitokeza jukwaani kule, na kuniambia nifanye jambo hilo. Nami nilifanya hivyo kwa neema Yake na rehema Zake. Mungu yeye yule aliyekuwa historia, wa miaka kumi iliyopita, amejitokeza jukwaani tena. Kwa hakika tu kama vile Yeye alivyotimiza jambo hilo, Yeye atalitimiza hili. Yeye ni Mungu wa historia, na Yeye ni Mungu wa siku hizi. Hasinzii wala kulala usingizi. Hawezi kufa, kwa maana hakuwa na mwanzo wala mwisho.

⁸⁹ Kwa upande wako, usiku wa leo, rafiki mwenye dhambi, hisia hiyo ndogo ya kutekenya iliyoko moyoni mwako, ambayo inakwambia kuwa Yeye ni yule yule, inayokwambia kuwa anaweza kukuweka huru kutoka kwa kila mzigo na kila uhalifu, na kila dhambi uliyomtenda.

⁹⁰ Unaweza kuweka matumaini yako katika nini? Sio hata nyumbani kwako, sio kwa mke wako, sio katika familia yako, mama au baba.

Matumaini yangu hayajajengwa juu ya kitu
chochote pungufu
Ya Damu ya Yesu na haki yake;
Wakati yote yanayoizunguka nafsi yangu
yakitoweka,
Basi yeye Ndiye tumaini langu lote na nanga.
Juu ya Kristo, Mwamba wenye imara,
tunasimama;
Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao.

⁹¹ Kanisa, rafiki, chochote kile, yote yanafikia mwisho wake. Lakini Yeye yu hai milele. Na kwa sababu Yu hai, sisi tunaishi pamoja Naye.

⁹² Ungetoa nini kwa kubadilishana? Unaweza kutoa nini? Vipi kama Mungu alikuwa usiku wa leo kujibu kwenye ile Hukumu? Ungefanya nini kuhusu hilo? Unaweka matumaini yako kwa taifa? Linavunjika, kama mengine yote. Ati unaweka matumaini yako katika uchaguzi fulani ujao? Hao watu, sina kitu dhidi yao, lakini ni watu wanaopatikana na mauti na wataondoka. Huwezi kuweka matumaini yako katika chochote hata kidogo, kitakachoshikilia, ila Mungu wa historia ambaye aliahidi angefufuka. Na siku fulani yenye baraka . . .

⁹³ Wanaweza kukupeleka kule na kukumwagia mavumbi, mtayarisha mazishi, lakini Mpeleka-juu atakuja huku moja ya siku hizi. Mtayarisha mazishi atakushusha chini, lakini Mpeleka-juu atakupeleka juu kwa uhakika tu. "Kwa maana wale waliokufa katika Kristo Mungu atawaleta pamoja Naye wakati atakapokuja." Kwa maana Yeye ni Mungu wa historia sasa, kwa wengi, lakini atakuwa Mungu wa siku hizi utakapomkubali kama Mwokozi wako na kumwona kuwa halisi moyoni mwako. Kutakuwa na kitu Fulani ndani yako kinachokwambia. Huenda usiwe na mhemko. Huenda usilie. Huenda usinene kwa lugha. Huenda usikimbie. Huenda usipige kelele. Lakini kitu fulani kitatukia, hata utajua, hata utajua ya kwamba jambo fulani limetukia. Maisha yako yatalingana moja kwa moja na hilo, maadamu ungali hai. Ndipo ile saa ya mwisho ikiwadia nawe uondoke humu duniani, hutaogopa mabaya. "Kwa maana Wewe upo pamoja nami. Gongo Lako na fimbo Yako, vitanifariji." Wakati daktari amekukatia tamaa, na kuondoka, na mishipa ya baridi inapanda.

⁹⁴ Kama Bw. Vauder hivi majuzi usiku, meya wetu mashuhuri wa zamani hapa jijini, alienda kumsikiliza Bw. Nixon akiongea, akafa pale pale. Mtu mzuri, mwenye afya, ni juavyo mimi.

⁹⁵ Nitaondoka nyumbani, nirudi, mke wangu kasema, "Billy, ulijua *Fulani-wa-fulani* alikufa?"

⁹⁶ Hivi majuzi, msichana wangu mdogo akiketi shuleni hapa juu, pamoja na msichana mdogo, Alhamisi, na Jumapili wakamzika. Alishikwa na nimonia. Ilingia moyoni mwake ama chochote kile, nao (yeye) ikamwua. Alikuwa amekufa.

⁹⁷ Naye rafiki yangu, Bibi Williams hapa, mke wa Buck William, nilimjua kwa miaka mingi. Zella Brakeman hapa, yuko hapa jengoni mahali fulani, ni dada yake, ambaye aliishi papa hapa, jirani, kwa miaka mingi, tulipoishi ng'ambo ya barabara. Akaondoka; kidogo alikuwa na wasiwasi, lakini alikuwa ameaga niliporudi.

⁹⁸ Mnaona ni kitu gani? Wakati mwingine, ni, utakumbana nayo. Na pesa zote unazoweza kukusanya, marafiki wote unaoweza kukusanya. . . Wote ni sawa. Lakini, hayo yote, acha hayo yawe ya pili. Mwamini Mungu wa historia, ya kwamba Yeye ni Mungu wa siku hizi, vivyo hivyo tu, uone kile atakachokufanyia.

⁹⁹ Kwenu ninyi mlio wagonjwa na wahitaji, daktari amekukatia tamaa na hawezi kukusaidia zaidi. Kumbukeni, Mungu wa historia ni Mungu yeye yule leo.

Hebu na tuombe kwa muda kidogo sasa, tunapoinamisha vichwa vyetu.

¹⁰⁰ Ikiwa kuna wale walio hapa usiku wa leo. . . sijui. Ikiwa kuna wale hapa ndani, usiku wa leo, wanaojua kwa ajili ya wokovu wa nafsi yako, kwamba kama yule Mungu aliyeahidi ya kwamba angekuja kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati hufikirii. Ikiwa huko pamoja Naye, unafikiria tu kuwa unaye, kumbuka, "Iko njia ionekanayo kuwa sawa, lakini mwisho wake ni njia za mauti." Kama huna uhakika kwamba—kwamba umeokolewa, usiku wa leo, na kama akija, ungeenda pamoja Naye, naomba ujitahidi na kumwinulia mkono wako, na kwa kufanya hivyo, useme—useme, "Unirehemu, Mungu." Asante. Mungu akubariki. Mikono mingi iliinuliwa. Je, kunaaweza kukawa na mwingine kabla hatujafunga? Je, wewe. . . na mwe na maombi. Mungu akubariki, ewe msichana. Usione aibu sasa. Hakika.

¹⁰¹ Kuna faida gani kumhubiri Mungu wa historia, kama si yeye yule leo? Na, ndugu, dada, nasema hivi. Nilisoma juu ya Mungu wa historia wakati mmoja. Nilisoma habari Zake kwenye vitabu. Nilisoma habari Zake katika Biblia. Lakini siku moja nikakutana Naye. Nilikutana Naye. Akanijia. Akaniambia nisinywe pombe, nisivute sigara wala—wala kujitia najisi, Naye alikuwa na jambo fulani kwangu kufanya nitakapokuwa mtu mzima kidogo. Nilikuwa mvulana mdogo tu. Yeye—Yeye alithibitisha hilo. Alifanya hivyo. Hii hapa picha Yake ikining'inia papa hapa sasa, wakati sayansi imeipiga. Mnaona? Ulimwengu unajua hilo. Amelithibitisha miongoni mwenu.

Anajua kila wazo moyoni mwako. Amejithibitisha Mwenyewe. Yeye ni Mungu yeye yule leo. Yeye si Mungu wa historia.

102 Usiwe ninii tu . . . usiache ulimwengu ukupake kisiri masizi na upuuzi wa ulimwengu. Mwamini sasa hivi . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Je, unaweza kuinua mkono wako? Wengine ambao hawajainua, unaweza kuinua mkono wako, useme, “Mungu, sina uhakika nalo, lakini nataka kuwa na uhakika. Nijalie. . .”

103 Mungu akubariki, kijana mwanamume. Mtu fulani? Na Mungu akubariki, hapo nyuma, dada. Mungu akubariki, ndugu. Mtu mwingine? Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki, hapo, ndugu. Hilo ni sawa.

104 Unasema, “Ndugu Bill, ingemaanisha lolote kwangu, kuinua mkono wangu?” Hebu inua mkono wako, wakati mmoja, uone. Sikuzote, ndugu, dada, unapofanya jambo lolote vema, unajisikia vizuri kulihusu.

105 Kuwa mwaminifu. Sasa, usimdanganye Mungu. Humdanganyi Mungu. Anajua. Unajidanganya mwenyewe. Unajua, uwongo mdogo ni jambo la kutisha sana, hata wanaweza kukupeleka katika mahakama za shirikisho na mahakama za jinai, na—na kuweka kigundua uwongo kwenye mkono wako, nawe unaweza kujaribu uwezavyo kusema jambo hilo, kulifanya lisikike kama ukweli, lakini mishipa yako itathibitisha kuwa unasema uwongo. Kwa nini? Hukuumbwa upate kusema uwongo. Na ikiwa kigundua uwongo kinajua, vipi kuhusu Mungu?

106 Unasema, “Lakini, ndugu, mimi ni Mbaptisti. Mimi ni Mpresbiteri. Mimi ni Mmethodisti.” Hiyo ni sawa.

107 Nakuuliza jambo moja. Je, umewahi kukutana na huyu Mungu wa historia? Je, Yeye amesimama kwenye kichaka kinachowaka moto mbele yako, nawe unajua? Naye akanena tena na nafsi yako, nawe unajua dhambi zako zimetoweka? Ikiwa sivyo, kamwe usibahatishe kwa kujiunga tu na kanisa, ama ulienda kule na kujisikia vizuri kidogo juu yake. Unapaswa kumjua Yeye. Sio kusikia habari Zake, si kupata baraka Zake, ni Uzima. Bali, kumjua Yeye, ni Uzima; kumjua, kumjua kibinafsi; Yeye, kiwakilishi nafsi, kumjua Yeye. Sio kukijua Kitabu Chake, sio kuwa mwanafunzi mzuri, sio kuwa mshiriki mzuri, ama mwanamume mwema ama mwanamke mwema. Hiyo hailifanyi; torati ilifanya hivyo. Lakini, kumjua Yeye! Je, umekutana Naye? Je, huyo Mungu, aliyenena na Musa katika kijiti kilichowaka moto, amekuja mbele yako? Je, umemsikia akinena nawe, mpaka ukajua ilikuwa ni Yeye? Kama hajafanya hivyo, inua tu mkono wako, useme, “Mungu, sema nami sasa. Je, huyo ni Wewe unayevuma kwenye moyo wangu? Na—nataka kukujua Wewe.”

108 Mungu akubariki, ewe msichana. Mungu akubariki, huko nyuma. Hilo ni zuri. Hiyo ni sawa. Mtu ambaye hana. Hiyo ni

sawa. Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki, ewe msichana, hapa. Hilo ni zuri. Mungu akubariki, ewe msichana hapa.

¹⁰⁹ Sasa kwa utulivu sana, huku vichwa vyenu vimeinamishwa, mkiuvumisha kwa upole.

Mapambazuko fulani yenye furaha, Yesu atakuja;
Mapambazuko fulani yenye furaha, vita vyote vilishindwa,
Tutapiga kelele za ushindi, tupenye kupitia anga za bluu,
Mapambazuko fulani yenye furaha, kwangu mimi, kwa ajili yako.

¹¹⁰ Sasa, ninyi mlioinua mikono yenu, kama kweli mnatamani maombi yangu kwa ajili yenu, na kuamini ya kwamba Mungu anenisikia, unataka kupanda hapa madhabahuni, hebu nisimame hapa niombe pamoja nawe, kidogo. Madhabahu iko wazi. Mungu akubariki, ndugu. Hiyo ni sawa. Mungu awabariki, wanaume. Mungu akubariki, dada. Simama moja kwa moja na upande juu. Ikiwa unaamini Mungu atakusaidia, na kusikia maombi, ili mimi nikusaidie uje Kwake, kumjua Yeye, njoo moja kwa moja sasa. Sivyoo?

Mapambazuko fulani yenye furaha, Yesu . . .

¹¹¹ Tunajuaje haitakuwa asubuhi?

. . .vita . . .

Vita hivyo unavyopigana sasa hivi, si utaviacha vishindwe sasa hivi, basi? Hebu vishindwe sasa hivi, ili uweze kupiga kelele za ushindi.

Mapambazuko fulani yenye furaha, kwa ajili yangu, kwa ajili yako.

Mapambazuko fulani yenye furaha, Yesu . . .

¹¹² Inuka tu moja kwa moja, hiyo ni kweli, na upande juu, huku.

. . .vita vyote vimeshindwa,
Tutapiga kelele za ushindi, tupenye kupitia anga za bluu,
Mapambazuko fulani yenye furaha . . .

¹¹³ Si utakuja sasa, tunapongojea? Tutakusaidia hapa, katika maombi. Maombi ya imani hutufanyia mengi. Hivi hutakuja? Ninakusihhi uje, umkubali Mungu wa wakati huu. Sio tu ki—kijimungu fulani, ambapo unaenda kanisani na kusema, “Vema, nilijiunga na kanisa.” Hicho kijimungu hakifai kitu. Mungu wa Kimethodisti, mungu wa Kibaptisti, mungu wa Kipresbiteri, mungu wa Kipentekoste, hawatafaa kitu. Mpate Mungu wa Biblia hii. Mungu wa Kipentekoste ataenda huko nje ulimwenguni; mungu wa Kimethodisti, ama mungu wa Kibaptisti, ama mungu mwingine yeyote wa kimadhehebu.

Lakini Mungu wa Biblia hii, atakufanya umpende Yesu. Hakika atakufanya. Roho Wake atakaa ndani yako, na maisha yako yote yatabadilishwa; hasira hiyo, ubaya huo, roho hiyo ya kutosamehe, kitu hicho kitakachotia doa nafsi yako katika Umilele uliopotea.

¹¹⁴ Ninapembeza tu wavu sasa. Ni juu yako. Ufuate ndani, sivyo? Sogeeni moja kwa moja, kuzunguka madhabahu hapa. Wengi wenu mliinua mikono yenu huko nyuma. Watu watawaruhusu msimame, karibu na viti vyao. Bwana akubariki, ewe kijana mwanamume.

¹¹⁵ Sasa wakati anacheza muziki kwa upole, hapa wamesimama kadhaa karibu na madhabahu. Watu saba waliokuja mbele kusimama kuzunguka madhabahu. Je, mnajua saba ni nambari kamili kwa Mungu, ukamilifu? Roho Mtakatifu ameshuka tu juu ya mtu anayesimama hapa, sasa hivi. Huyu ndiye ninayemwita Roho Mtakatifu, ndugu.

¹¹⁶ Sasa Yeye yuko hapa, kwa kila mmoja wenu. Iweni tu wanyenyekevu mioyoni mwenu. Vipi kama hii ilikuwa ndiyo mara ya mwisho ungewahi kusimama karibu na madhabahu, hii ndiyo sala ya mwisho uliyowahi kusema, sasa hivi? Yesu atakuja. Anaweza kubisha mlangoni pako kabla ya asubuhi, unajua. Huna budi kwenda, siku moja, kama Yeye ni Mungu wa yote. Yeye ni Mungu wa historia, na Yeye ni Mungu wa siku hizi.

¹¹⁷ Alizungumza nawe. Umesimama hapa mbele Zake, kukutana Naye. Umekuja mbele kukutana Naye. Atakutana nawe. Amesimama papa hapa sasa. Moyoni mwako tu, ungama yote ambayo umefanya ambayo ni makosa. Useme “Mungu, unirehemu mimi mwenye dhambi. Nimefanya kosa na—na sasa ninakiri, kwa moyo wangu wote, kwamba nimekosea. Nataka unirehemu na unisamehe dhambi zangu. Ni—nitakutumikia siku zangu zote. Na hebu moto huu mdogo unaowaka moyoni mwangu, imani ndogo, iliyonifanya nije hapa kwenye madhabahu hii, usiku wa leo, jalia iingie chini kabisa nafsini mwangu. Jalia ishike papa hapa sasa. Na kitu kiwake moto, ambacho kinaniambia tu, ‘Naam, U hai, Yesu.’ Nami nakupenda. Nami nitakuona jukwaani katika saa chache zijazo, ukifanya mambo, mambo makuu. Nina furaha sana kwamba nilikuja mbele ulipozungumza na moyo wangu. Nitakuona ukifanya kansa iwaache watu, ukiwaponya wagonjwa na wahitaji. Tuwasikie wakirudi, wakishuhudia yale Mungu aliyowatenda; Mungu wa historia, ambaye ameinuka juu kutoka katika historia, naye ni yeye yule leo, anakuja jukwaani. Kwa sababu, Yeye anakuja wakati huu kukaa; Kuja Kwake mara ya pili.”

Hebu tuombe sasa. Ombeni pamoja nami, kila mmoja wenu.


¹¹⁸ Mungu Mpendwa, ninaleta mbele Yako sasa hivi, hawa saba. Usiku wa kwanza ulitoa nyota saba zinazotangatanga. Umesea, katika Neno Lako la thamani, “Hakuna mtu awezaye

kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Naye anijiaye Mimi, sitamtupa nje kamwe, bali nitampa Uzima wa Milele, nami nitamfufua siku ya mwisho.” Bwana, hiyo ni ahadi Yako. Na kwa mhemko, hatua ya kusadikisha, nafsi hizi saba za thamani zinazotangatanga zimesonga mbele usiku wa leo, kwa sababu wanaamini ya kwamba Mungu yule aliyenenwa na manabii, Mungu yule aliyenena na yule kipofu, angali anaishi leo. Nao wamesonga mbele kukutana Naye.

¹¹⁹ Mungu yeye yule aliyetoa ile ahadi, na kukutana na mwenye ukoma kwa misingi yake mwenyewe, ambaye alikutana na yule mwanamke mwenye kutokwa na damu ukingoni mwa mto, ambaye alikabiliana na mauti kwenye kaburi la Lazaro na kumgeuza tena, ni Mungu yeye yule usiku wa leo, ambaye anasimama hapa kukabiliana na mauti haya ya kiroho na kumgeuza. Na kusema, “Ondoa mikono yako kutoka kwa hawa ambao wamekuja kunikiri Mimi kwa kuvutwa na Roho Wangu. Nitawapa Uzima wa Milele, wala hakuna mtu awezaye kuwaondoa Kwangu. Nitawafufua katika siku za mwisho.”

¹²⁰ Tunakushukuru kwa ajili yao, Baba. Na tunaomba kwamba watadumu waaminifu mikononi Mwako, mpaka mauti itakapowaweka huru. Watakapoingia katika furaha za Bwana, kwenye siku ile kuu, wakati Karamu ya Arusi itakapoandaliwa kote angani, ambapo Mfalme atatoka na kusema, “Unakumbuka siku ile ya kwanza ya Oktoba, 1958, kwenye ile maskani ndogo ya zege? Ulitembea na kunichukua Mimi kama Mwokozi wako. Nilizungumza na wewe. Ulikuwa mwenye dhambi wakati huo, lakini sasa nilikuokoa. Na sasa wewe ni Wangu, nawe unao Uzima wa Milele. Sasa ingia katika furaha ambazo nimekuandalia, tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Tujalie, Bwana. Wao ni Wako sasa. Tunawakabidhi Kwako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Sasa huku vichwa vyenu vimeinamishwa, enyi kusanyiko.

¹²¹ Nitawauliza kila mmoja wenu hapa madhabahuni. Je, unahisi, chini moyoni mwako sasa, kutoka kwenye kilindi cha nafsi yako, kwamba ule mwali mdogo wa imani uliokwambia uje mbele madhabahuni hapa, kutenda tendo hili ulilofanya sasa, baada ya kuinua mikono yako na kuja mbele, unahisi kwamba mwali huo mdogo umeanza kuwaka kuelekea imani halisi iliyo hai moyoni mwako? Na sasa unaamini ya kwamba Yesu amekusamehe dhambi zako, nawe utakuwa Wake tangu sasa na kuendelea? Kama unaamini, je, waweza kumwinulia mkono wako wa kuume? Wale waliozunguka madhabahu, inua mkono wako wa kuume, kama unahisi kwamba Yesu amekusamehe dhambi zako zote. Wale walio karibu... Sasa, kuna mikono miwili, mitatu, haijainuliwa. Sasa endeeleni tu kuomba, kila mtu. 

58-1001 Kumwinua Juu Kutoka Katika Historia
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org